

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO

KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MENEJIMENTI YA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO KILICHOFANYIKA TAREHE
20 OKTOBA, 2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO.

A: WAJUMBE:

- | | |
|----------------------------|---|
| 1. Ndg. Gastone Missungwi | - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) – Mwenyekiti |
| 2. Ndg. Shadrack P. Msungu | - Kaimu Afisa Utumishi na Utawala (W) - Katibu |
| 3. Ndg. David Sichizya | - Kaimu Afisa Habari (W) |
| 4. Ndg. Gerson Mshana | - Kaimu Mhandisi Ujenzi (W) |
| 5. Ndg. Shams Abdalah | - Kaimu Kaimu Mganga Mkuu (W) |
| 6. Ndg. Sijali Marco | - Afisa Usafirishaji |
| 7. Ndg. Nkandala Enos | - Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 8. Ndg. Mussa J. Mlonga | - Kaimu Afisa Misitu (W) |
| 9. Ndg. Dorothea Malima | - Meneja CPU |
| 10. Ndg. Jojujo Chimweta | - Kaimu Afisa Usafishaji na Mazingira (W) |
| 11. Ndg. Vedastus Msiba | - Kaimu Katibu TSC |
| 12. Ndg. Gelasius Ngaya | - Kaimu Mthibiti Ubora wa Shule (W) |
| 13. Ndg. Christina Mhina | - Kaimu Afisa Mipango (W) |
| 14. Dr. Elfes Msenya | - Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 15. Ndg. Vicent Bushaija | - Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 16. Ndg. Kurwa Hanta | - Kaimu Afisa Ardhi na Mazingira (W) |
| 17. Ndg. Aisha Kesowani | - Mratibu TASAF |
| 18. Ndg. Geriad Mgoba | - Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 19. Ndg. Mlingwa Methusela | - Kaimu Mwanasheria (W) |
| 20. Ndg. Fransisca Charles | - Afisa Afya |
| 21. Ndg. Rashida Laiser | - Kaimu Afisa Manunuzi (W) |
| 22. Salvatory Mlingi | - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 23. Ndg. Emmanuel Kwezi | - Mwandishi wa Vikao |
| 24. Ndg. Alodia Eugen | - Mwandishi wa Vikao |

MUHT.NA .01/20/10/2021 – KUFUNGUA KIKAO:

Katibu wa kikao alimkaribisha Mwenyekiti wa timu ya Menejimenti kwa ajili ya kufungua kikao baada ya akidi ya Wajumbe kutimia.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 04:24 Asubuhi.

MUHT.NA.02/20/10/2021 – KUTHIBITISHA AJENDA ZA KIKAO:

Ajenda **zilizothibitishwa** kwa ajili ya kikao hicho ni kama zilivyo katika muhtasari huu.

MUHT.NA.03/20/10/2021 – KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TEREHE 10/09/2021:

Muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 10/09/2021 **ulisomwa, ukathibitishwa na kupokelewa**, na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao husika.

MUHT.NA. 05A (iv)/ 20/10/2021 – TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSH. 3,750,000,000.00 KWA AJILI YA UJENZI WA VYUMBA 183 VYA MADARASA NA UJENZI NYUMBA YA WATUMISHI (THREE IN ONE) ZAHANATI YA MNEKEZI

Iliwasilishwa taarifa kuwa Halmashauri ilipokea fedha za UVIKO 19 Tsh.3,750,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 183 vya madarasa. Kwa mchanganuo ufuatao:-

- Shule za Sekondari kujenga madarasa 151 kwa thamani ya Tsh.3,020,000,000.00.
- Shule shikizi za Msingi kujenga madarasa 32 kwa thamani ya Tsh.640,000,000.00
- Nyumba ya Watumishi (Three in One) Zahanati ya Mnekezi Tshs. 90,000,000.00

Wajumbe **walipongeza na kushukuru** juhudi kubwa za mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa Taifa pia na kwa kuipatia Wilaya ya Chato fedha za ujenzi wa madarasa (UVIKO 19 na Ujenzi wa Nyumba ya Watumishi).

Taarifa ilipongezwa, kupokelewa na kukubaliwa.

MUHT.NA.06/20/10/2021 – KUAHIRISHA KIKAO:

Akifunga kikao, Mwenyekiti Alishukuru Wajumbe kwa majadiliano mazuri ya taarifa mbalimbali. Alisisitiza kila Idara yenye vyanzo vya mapato kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato.

Mwenyekiti aliahirisha kikao saa 05:44 Asubuhi.

TUNATHIBITISHA KUWA HII NI SEHEMU YA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CMT MUHT.NA. 05A (iv)/ 20/10/2021 – TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSH.3,750,000,000.00 KWA AJILI YA UJENZI WA VYUMBA 183 VYA MADARASA NA NYUMBA YA WATUMISHI (THREE IN ONE):

KUSAINI NA:-


KATIBU
6/6/2022
TAREHE


MWENYEKITI
6/6/2022
TAREHE

2

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S. L. P. 116
CHATO